

CHACHANDU CHACHU

- | | |
|--|--|
| <p>1. Chachandu iliyochacha, sio chachandu chachizi.
Huuchachuza mchicha, na kuchachiza mchuzi.
Huchuruza kwe? pakacha, churuzi ya uchirizi.
Huchachizia mchuzi, chachandu iliyochacha.</p> <p>2. Chachandu iliyochacha, hutaghayari churuzi.
Uonjapo utaacha, kwa kuchelea ushuzi.
Utashinda kutwa, kucha, kwa kula viso ujuzi.
Huchachizia mchuzi, chachandu iliyochacha.</p> <p>3. Chachandu iliyochacha, walo huziba tuzi.
Matumbo yao huchacha, kupenda vya upuuzi.
Tamathali ya machicha, chujo la tui na nazi.
Huchachizia mchuzi, chachandu iliyochacha.</p> | <p>4. Je, tungo za kuparacha, mithibali iliyo wazi.
Waliopo ni mapicha, fasihi hawaziwezi.
Huparurana makucha, kwa tungo za ubazazi.
Huchachizia mchuzi, chachandu iliyochacha.</p> <p>5. Tungo zao parakacha, mwaziona wazi wazi.
Mhariri aziacha, audodesha utunzi.
Si tungo bora kuacha, mnaleta uchafuzi.
Huchachizia mchuzi, chachandu iliyochacha.</p> <p>6. Tamati beti naziacha, enye weledi wa enzi.
Nalonga bila kuficha, makinda hawaniwezi.
Safu hii watakacha, warande kama machizi.
Huchachizia mchuzi, chachandu iliyochacha.</p> |
|--|--|

*Ustadh Rashid I.M. Mkwinda (Ngominenga)
Kilwa Kivinje.*

*(Limetoka kwenye Mwananchi, Jumanne Julai 23,
2002, uku.20)*